NYIC

Updated: 2024.12.13
SWAHILI

# Uwepo wa Maafisa wa Uhamiaji katika Mahali pa Kazi



**Mwongozo huu utaeleza maafisa wa uhamiaji ni nani, nini cha kufanya ikiwa watafika kwenye mahali pako pa kazi, na namna ya kuwa tayari ikiwa kuna uvamizi.**

## ICE ni nini?

- ICE ni kifupi cha Immigration and Customs Enforcement (Wakala wa Utekelezaji wa Sheria za Uhamiaji na Forodha), wakala wa serikali ya shirikisho chini ya Wizara ya Usalama wa Ndani (Department of Homeland Security [DHS]) inayosimamia sheria za uhamiaji.
- Maafisa wa ICE ni maafisa wa serikali ya shirikisho, na si sawa na polisi. Sare zao huweza kusema “Police,” “Federal Agent,” “ICE,” au “HSI.” Pia wanaweza kuvaa nguo za kiraia. Wanaweza kubeba bunduki vilevile. Wakati mwingine, polisi wanaambatana na maafisa wa ICE katika uvamizi wa ICE.

## Maafisa wa ICE wanafanya nini kwenye mahali pa kazi?

- Maafisa wa uhamiaji wanaweza kuja kwenye mahali pako pa kazi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa Fomu I-9; kufanya uvamizi; au kuwaweka kizuizini watu fulani.

## Kuna tofauti gani kati ya ukaguzi (audit) na uvamizi (raid)?

- Uvamizi wa ICE unapotokea, mwajiri huwa hana taarifa. Ikiwa ni ukaguzi, mara nyingi mwajiri hupewa hati ya mahakama kabla. Ukaguzi wa ICE ni “mpole” zaidi kuliko uvamizi, lakini zote mbili zinaweza kupelekea matokeo mabaya.

## Fahamu Haki Zako wakati wa kutembelewa au kuvamiwa na ICE

- Mara zote una haki ya kukaa kimya na kutojibu maswali.
  - Taarifa yoyote unayowapa maafisa wa ICE inaweza kutumika dhidi yako badaaye.
  - Unaweza kusema, “Nataka kukaa kimya” (I want to remain silent) au “Sitaki kujibu maswali” (I don’t want to answer questions).
- Mara zote una haki ya kukataa kupekuliwa wewe na mali zako.
  - Huhitaji kuwaonesha maafisa wa ICE kitambulisho chochote wala nyaraka zozote. Kila mtu ana haki hii.
  - Unaweza kusema, “Sikupi ruhusa ya kunipekua” (I do not consent to a search).
- Maafisa wa ICE hawawezi kumweka mtu yeyote kizuizini au kuingia maeneo ya faragha bila hati ya mahakama.
- Mara zote una haki ya kuwarekodi maafisa wa ICE na matendo yao, ili mradi tu kwamba huingilii kazi yao.

# WAFANYAKAZI: Jinsi ya kuwa tayari kwa ujio wa ICE

## Kabla ya ujio wao


- Kuwa tayari kwa kitu kibaya kutokea.
    - Ongea na mwanasheria wa uhamiaji, au tumia muda wako kumtafuta mwanasheria.
    - Kuwa na mpango wa usalama wa familia na kuwatunza watoto.
    - Shika namba muhimu za simu kichwani.
    - Tunza vizuri nyaraka muhimu.
    - Kuwa na akiba ya pesa kwa matumizi ya dharura.
    - Ikiwezekana, hudhuria warsha ya Fahamu Haki Zako (Know Your Rights) na washirikishe wafanyakazi wenzako ulichojifunza.
- Fahamu haki zako ni zipi kutegemeana na maeneo uliyopo kwenye mahali pako pa kazi:
    - Maeneo ya Umma
        - Maeneo ya umma ni maeneo ambayo mtu huweza kuingia bila ruhusa.
            - Mfano: sehemu ya kulia chakula katika mgahawa; eneo la manunuzi la supamaketi; eneo la kuegesha magari; eneo la mapokezi la jengo la ofisi.
        - Maafisa wa ICE wanaweza kuingia maeneo ya umma ya mahali pa kazi bila ruhusa.
        - Maafisa wa ICE hawawezi kumsimamisha, kumhoji, au kumkamata mtu yeyote kwa sababu pekee ya kuwa kwenye maeneo ya umma.
    - Maeneo ya Faragha
        - Hakuna mtu anayeweza kuingia maeneo ya faragha ya mahali pa kazi bila ruhusa ya mwajiri au hati ya mahakama.
        - Maafisa wa uhamiaji wanaweza kudai kuingia maeneo ya faragha ikiwa wana hati ya mahakama tu.
    - Tengeneza mpango na wafanyakazi wenzako na mwajiri wako. Fahamu maeneo gani ya mahali pako pa kazi ni ya umma na maeneo gani ni ya faragha.
- Fahamu Haki Zako!
    - Una haki ya kukaa kimya na kutojibu maswali yoyote.
    - Huhitaji kuonesha kitambulisho chako.
    - Una haki ya kukataa kupekuliwa wewe na mali zako.
    - Una haki ya kutowekwa kizuizini bila sababu halali.
    - Una haki ya kuwarekodi maafisa wa dola.

## Wakati wa ujio wao

- Tulia. Usiwakimbie maafisa au kujificha. Ukifanya hivyo, inaweza kuwapa sababu ya kukukamata.
- Waelekeze maafisa wote na maswali yao yote kwa msimamizi wako au mwajiri wako.
- Usiongee na afisa yeyote. Kitu chochote unachosema kinaweza kutumika dhidi yako au dhidi ya wafanyakazi wenzako.
    - Huhitaji kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji, mahali unapotoka, au umekuwa Marekani kwa muda gani.
    - Huhitaji kujibu maswali kuhusu waajiriwa wengine.
- Ikiwa maafisa wa ICE wanajaribu kuingia maeneo ya faragha, unaweza kumwambia: “Hili ni eneo la faragha. Huwezi kuingia bila hati ya mahakama inayosainiwa na hakimu” (This is a private area. You cannot enter without a judicial warrant signed by a judge), na kuwaelekeza kwa msimamizi wako au mwajiri wako.
- Tazama maafisa wanafanya nini na ukijisikia salama, urekodi video ya matendo yao.

## Baada ya ujio wao

- Andika taarifa zote unazokumbuka zikiwemo:
    - Taarifa za maafisa kama majina yao na namba zao za utambulisho,
    - Jinsi wanavyoonekana:
        - Walivyofanya matendo yao na walivyosema maneno yao.
        - Walivaa nguo au sare gani, na kama walibeba silaha.
        - Walivyowatendea waajiriwa wote.
- Ripoti uvamizi wa ICE kwa shirika la kijamii linaloaminika au chama cha wafanyakazi, iwapo unaweza.



# WAAJIRI: Jinsi ya kuwa tayari kwa ujio wa ICE

## Uvamizi wa ICE

- Maafisa wa ICE wanaweza kwenda mahali pa kazi bila onyo au kutoa taarifa yoyote, kama ni sehemu ya kumchunguza mwajiri.
- Maafisa wa ICE wanaweza kufika kwenye biashara yako na kujaribu kumpata mtu (au watu) fulani. Wakati wa kuwepo, wanaweza kujaribu kuwahoji, kuwaweka kizuizini, na hata kuwakamata watu wengine.
- Maafisa wa ICE wanaweza kujaribu kumsimamisha, kumhoji, au hata kumkamata mfanyakazi bila madaraka halali.

## Kaguzi 1-9

- Fomu I-9 inahitajika kwa wafanyakazi wote wapya.
- Ukaguzi wa Fomu I-9 ni pale ambapo ICE wanakuja kwenye eneo lako la biashara kukagua kama umefuata matakwa ya Fomu I-9.
- Fomu I-9 inahakiki utambulisho wa mfanyakazi na uhalali wa kufanya kazi Marekani.
- Kama mambo yakienda kombo:
  - Ikiwa ICE wakiamua kwamba biashara haikufuata matakwa ya Fomu I-9, yafuatayo yanaweza kutokea:
    - Zuio la kuajiri bila kuwa na vibali halali vya kazi.
    - Faini na adhabu za madai na jinai.
- ICE inaweza kumweka mfanyakazi fulani kizuizini kwa sababu ya hali ya Fomu I-9 yake.

## Kabla ya ujio wao

- Andika mpango wa nini cha kufanya mapema kabisa
  - Zungumza na biashara au taasisi zingine. Waulize wanajiandaaje.
  - Andaa mpango unaokufaa wewe.
  - Fanya jaribio – kama vile kuona nini cha kufanya moto unapotokea. Utakuwa tayari zaidi ukishazoea nini cha kusema na kufanya.
  - Jiunge katika mitandao ya mashirika yanayohusiana na uhamiaji katika eneo lako. Wanatoa msaada wa kifamilia, kisheria, kifedha na maswali yanayohusiana na usambazaji wa taarifa katika vyombo vya habari pale ambapo maafisa wa uhamiaji wanapotembelea biashara yako.
- Wafundishe wafanyakazi wako wasizungumze na maafisa wa ICE.
  - Wafundishe wafanyakazi wasiwaruhusu maafisa wa ICE kuingia eneo la kazi.
  - Mfanyakazi anaweza kusema, “Siwezi kukupa ruhusa ya kuingia. Ni lazima uongee na mwajiri wangu.”
  - Wafundishe wafanyakazi wote wasizoeane na maafisa wa ICE. Ikiwa maafisa wa ICE wana maswali au matakwa fulani, wafanyakazi wasizungumze chochote, au wanaweza kusema, “Huruhusiwi kuingia. Zungumza na mwajiri wangu.”
- Fahamu Haki Zako!
  - Waajiri wana haki wanapotembelewa na ICE. Maafisa wa ICE hawana haki mara zote za kuingia kwenye eneo lako la biashara, kuwasimamisha au kukamata wafanyakazi wako, au kuchukua nyaraka.
  - Fanya kazi na kundi la jamii au la kisheria ili kuandaa warsha ya “Fahamu Haki Zako” kwa ajili yako na wafanyakazi wako na uwalipe wafanyakazi wako kwa muda wanaotumia katika mafunzo.
  - Fahamu tofauti ya hati ya mahakama na hati ya utawala
    - Hati ya mahakama lazima isainiwe na hakimu na iseme “U.S. District Court” au itaje jina la mahakama ya jimbo kwa juu.
      - Hati ya mahakama inasainiwa na hakimu wa jimbo au serikali ya shirikisho.
      - Hati ya mahakama inaweza kuwapa maafisa wa chombo cha dola ruhusa ya kuingia maeneo ya faragha kama nyumbani kwa mtu, au kukagua gari.
      - Bila kuwa na hati ya mahakama, maafisa wa ICE wanahitaji ruhusa ya kuingia katika maeneo ya faragha ya biashara yako.
      - Mifano: Hati ya Kukamata, Hati ya Upekuzi
    - Hati ya utawala inasainiwa na afisa wa DHS na siyo hakimu.
      - Haiwapi maafisa wa ICE au CBP mamlaka yoyote ya kuruhusiwa kuingia katika maeneo ya faragha ya makazi au eneo la kazi.
      - Mifano: Hati ya Kumkamata Mgeni, Hati ya Kuondoa/Kumtoa Mtu Nchini kwa Nguvu

# WAAJIRI: Jinsi ya kujiandaa na ujio wa ICE

## Wakati wa ujio huo

- Tulia! Waelekeze wafanyakazi wako watulie pia. Usikimbie na kutoka nje. Kufanya hivyo, kutafanya mambo yawe mabaya zaidi kwani maafisa wa ICE wanaweza kusema kwamba watu wanaokimbia wanaweza kuwa wamevunja sheria za uhamiaji.
- Iwapo maafisa wa ICE watajaribu kuingia katika eneo la faragha, unapaswa kusema: “Hili ni eneo la faragha. Huwezi kuingia bila ya kuwa na hati ya mahakama iliyosainiwa na hakimu. Je, una hati ya mahakama?”
  - USHAURI: Ili kuonesha kuwa eneo fulani ni eneo la faragha, unaweza kuweka nembo mlangoni linalosema “FARAGHA” (Private), huku ukiwa umerudishia mlango au kuufunga kwa ufunguo, na kuwa na sera kwamba wageni na watu wasiofanya kazi hapo hawawezi kuingia maeneo hayo bila ruhusa.
- Afisa wa ICE akikuonesha hati ya utawala iliyo na jina la mwajiriwa:
  - Huhitaji kusema kama mfanyakazi huyo yupo kazini siku hiyo au la.
  - Huhitaji kuwapeleka maafisa wa ICE kwa mfanyakazi waliyemtaja kwenye hati hiyo (hata kama yuko kazini siku hiyo).
- Usiwasaidie maafisa wa ICE kufahamu hali ya uhamiaji ya wafanyakazi wako au nchi wanazotokea.
- Watazame maafisa hao kuona kama wanafuata yaliyoandikwa kwenye hati.
- Iwapo wewe au mfanyakazi wako wana utayari, rekodi video inayoonesha maafisa wa ICE wanachofanya wakiwa katika eneo lako la kazi. Hii inaweza kukusaidia kuonesha kwamba maafisa walikiuka haki zako au za wafanyakazi wako.




## Baada ya ujio wao

- Andika au rekodi vitu hivi baada ya maafisa wa ICE kuondoka:
  - Je, kulikuwa na maafisa wangapi wa ICE (ndani na nje)?
  - Je, maafisa walikuwa wamevaaje? Walikuwa na silaha?
  - Je, maafisa walikufanya wewe au wafanyakazi wako kudhani kwamba hamwezi kusogea au kuondoka?
- Je, walimdhalilisha mtu yeyote? Kama ndiyo, kivipi?
- Kifahamishe chama cha wafanyakazi, iwapo unaweza.
- Ikiwa ICE watamkamata mfanyakazi wako yeyote, waulize wanampeleka wapi. Taarifa hii itaisaidia familia na mwanasheria wa mfanyakazi huyo kuweza kumpata.
- Toa taarifa ya uvamizi.
- Iwapo mtu amewekwa kizuizini, cheki mtandaoni kwenye mtandao wa ICE unaoonesha watu waliowekwa kizuizini locator.ice.gov

### Rasilimali

- Unaweza kupata orodha nzima ya rasilimali mbalimbali za Fahamu Haki Zako katika lugha mbalimbali hapa: nyic.org/kyr
- Kwa taarifa zaidi kuhusu haki za wahamiaji na jinsi ya kujilinda kama jamii, tembelea : immigrantdefenseproject.org
- Kwa taarifa zaidi kuhusu huduma za kisheria kwa ajili ya jamii za wahamiaji, tembelea Kituo cha Kitaifa cha Sheria ya Uhamiaji : nilc.org/resources/
- Ikiwa unahitaji msaada na kesi yako au ikiwa una swali la jumla kuhusu uhamiaji, piga simu Ofisi ya New Americans 1-800-566-7636 au tembelea tovuti yao: dos.ny.gov/office-new-americans